Zana Bora za Uzalishaji wa Ngano: Mwongozo wa Mafunzo kwa Wakulima na Wafanyakazi wa Ugani, Afrika Mashariki

Abstract:

Uzalishaji duni wa ngano miongoni mwa wakulima wadogo nchini Kenya na Tanzania umehusishwa na changamoto na vikwazo mbalimbali vinavyowakabili wakulima hao. Vikwazo hivyo ni pamoja na kutopatikana na gharama kubwa za huduma za zana na mashine, magugu korofi, wadudu na ma- gonjwa ya mimea, gharama kubwa za pembejeo, mifumo duni ya mbegu, mbinu duni za usimamizi wa udongo na maji, kiwango kidogo cha ujuzi na upatikanaji wa taarifa kuhusu mbegu mpya na zili- zoboreshwa, pamoja na udhaifu wa taasisi katika mnyororo wa thamani. Ikilinganishwa na wakulima wakubwa, wakulima wadogo wanachukuliwa kuwa wazalishaji wasio na tija na hivyo kushindwa kun- ufaika kikamilifu kutokana na ushiriki wao dhaifu katika mnyororo wa thamani wa ngano. Hii inaashiria kwamba wakulima wadogo wanahitaji maarifa na ujuzi wa ukulima ufaao pamoja na teknolojia za gharama nafuu na zinazoweza kufikiwa ambazo ni rafiki wa mazingira yao na zinazo ongeza tija.